# KATIKA MAFUNDISHO YANAYOTOKANA NA SAFARI TUKUFU YA KUHAMA KWA MTUME S.A.W

## NI MIPANGO NA KUTEGEMEA UWEZo

Imefasiriwa na

Profesa.Ayman Alasar

**Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa viumbe vyote, mwenye kusema katika Kitabu chake Kitukufu: {Ikiwa nyinyi hamtamnusuru Mtume, basi Mwenyezi Mungu alikwisha mnusuru walipo mtoa walio kufuru, naye ni wa pili katika wawili walipo kuwa katika pango, naye akamwambia sahibu yake: Usihuzunike. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi. Mwenyezi Mungu akamteremshia utulivu wake, na akamuunga mkono kwa majeshi msiyo yaona, na akalifanya neno la waliokufuru kuwa chini, na Neno la Mwenyezi Mungu kuwa ndilo juu. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye nguvu Mwenye hekima}. Ninashuhudia kuwa hakuna Mola wa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake asiye na mshirika. Na ninashuhudia kuwa bwana wetu na Mtume wetu Muhammad S.A.W ni mja wake na Mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu mteremshie sala salamu na baraka kwake na kwa watu wake na Maswahaba zake na wale wote waliowafuata kwa wema mpaka siku ya malipo.**

**Baada ya hayo:**

**Safari tukufu ya kuhama Mtume S.A.W kutoka Makka kwenda Madina ni yenye kujaa masomo mafundisho na mazingatio, kwani safari hiyo ni nukta kubwa ya mabadiliko katika historia ya Uislamu, miongoni mwa mafundisho muhimu ambayo yanapaswa kujifunza nayo ni mipango imara na mpangilio wa kina wa safari hii tukufu, kwani mipango ni hatua ya vitendo ili kuvuka matatizo mbali mbali lakini ni muhimu katika mafanikio, hilo linaonekana wazi pale Mtume S.A.W alipoandaa vipando viwili kwa ajili ya safari tukufu, na akamteua Ababakri R.A wa kufuatana naye kwenye safari hii, kama vile Mtume S.A.W aliteua muda wa usiku kwa kuwa ni wakati sahihi wa kutoka mji wa Makka.**

**Kama vile mwenye kuzingatia matukio ya kuhama kwa Mtume S.A.W ataona ni namna gani Mtume S.A.W aligawa majukumu kwa ukina zaidi pale alipomtaka Ally Ibn Abitwalib R.A kulala kwenye kitenda chake Mtume S.A.W akiwa amejifunika shuka ya Mtume S.A.W pia kurejesha amana za watu kwa wenyewe, na washirikina washindwe kumfuatilia Mtume S.A.W wakati wa kutoka kwake.**

**Ni wazi pia umuhimu alioutoa Mtume S.A.W kwa kuweka mipango madhubuti na kuchukuwa sababu za safari tukufu pale Mtume S.A.W alipokwenda kwa rafiki yake Ababakri R.A ndani ya wakati ambao**

**hakuwa na mazoea Mtume kwenda ndani ya wakati huo ili watoke wakiwa wenye kuhama baada ya kumpa jukumu Abdillah Ibn Abibakri R.A kufuatailia na kuwachunguza makuraishi ili kufahamu yale wanayopanga miongoni mwa vitimbi kwenye msafara huu wa kuhama, nyakati za mchana alikuwa anasikiliza mipango ya makuraishi na nyakati za usiku alikuwa anakwenda kulala alipo Mtume S.A.W na rafiki yake katika pango, kisha asubuhi anarudi Makka kwa mara nyengine.**

**Kama vile Abubakri R.A alimwandaa mtumishi wake Amiri Ibn Fahirah R.A ili kuwapelekea chakula kupitia kazi ya uchungaji wa wanayama wake karibu kabisa na pango lakini pia wanyama wale kufuta athari za nyayo za Abdillah Ibn Abibakri kwa kutumia kwato zao, pembezoni mwa hili Bibi Asmaa binti Abibakri R.A alikuwa amepasua njia yake ya kuelekea kwenye pango ili kupeleka chakula kwa Mtume S.A.W pamoja na rafiki yake R.A.**

********

**Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu Mola mlezi wa viumbe vyote, swala na salamu zimwendee Mtume wa mwisho naye ni Mtume Muhammad S.A.W pamoja na watu wake na Maswahaba wake wote.**

**Miongoni mwa mafunzo muhimu kwenye safari hii tukufu ya Mtume S.A.W ni pamoja na kutegemea uwezo ili kutekeleza majukumu**

**ambayo yanakubaliana na uwezo wao, ambapo Mtume S.A.W na rafiki yake Abubakri R.A walimpa kazi mtu ya kuwaelekeza njia ya kwenda Madina kwa kutumia njia zisizo zoeleka, naye alikuwa ni Abdillah Ibn Uraiqatw, hakuwa Muislamu lakini hata hivyo aliangukia kuteuliwa na Mtume S.A.W kwa kuaminika kwake kuwa na uwezo na kuwekeza nguvu zake hata kuwe na tafauti ya mitazamo au imani, kutoka kwa Mama wa Waumini Aisha R.A amesema: "*Mtume S.A.W na Abubakri walimpa kazi mtu…muongozaji…..wakamuamini, wakamtaka aandae vipando viwili na kuwafuata katika pango baada ya siku tatu akiwa na vipando hivyo asubuhi ya siku ya tatu, wakatoka wakiwa na Amiri Ibn Fuhairah na muongozaji na wakachukuwa njia ya pande za fukwe*".**

**Yote haya yanatufundisha umuhimu wa kuchukuwa sababu kwa kuweka mipango mizuri na kutegemea uwezo kwenye mambo yote, na hasa katika mambo mazito, na hilo halipingani na ukweli wa kumtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kama Mtume S.A.W angependa kumuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu kumbeba kwa kutumia mnyama buraku kutoka Makka kwenda Madina lakini pamoja na uelewa wake kamili kwa Mola wake na imani yake kubwa ya ushindi wake anatufundisha Mtume S.A.W kuchukuwa sababu, na kufanya maandalizi kwa kila jambo, kisha matokeo yake tunamwachia Mwenyezi Mungu Mtukufu akadarie vile atakavyo, na linaonekana**

**hilo wazi pale Mtume S.A.W alipochukwa sababu zote za mafanikio na ushindi, kisha akasema kumwambia rafiki yake Abibakri R.A pale walipokuwa wanafukuzwa na washirikina: {Usihuzunike kwani Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi} Mwenyezi Mungu Mtukuf akamlipa Mtume wake: {Mwenyezi Mungu akamteremshia utulivu wake, na akamuunga mkono kwa majeshi msiyo yaona, na akalifanya neno la waliokufuru kuwa chini, na Neno la Mwenyezi Mungu kuwa ndilo juu. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye nguvu Mwenye hekima}.**

**Ewe Mwenyezi Mungu tuwezeshe ufuasi mzuri kwa Mtume wako S.A.W**